*Mulika, Na. 44 (1), 1-13*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Usomaji wa Riwaya ya *Fanani* ya Zainab Baharoon kwa Kuzingatia Mawazo ya Mikhail Bakhtin

*Kyallo W. Wamitila*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.1

**Ikisiri**

Makala haya yamechunguza riwaya ya *Fanani* iliyoandikwa na Zainab Alwi Baharoon kwa kuongozwa na misingi ya Nadharia ya Usemezano inayohusishwa na mhakiki wa Kirusi, Mikhail Mikhailovich Bakhtin. Msingi na kichocheo kikuu cha uchunguzi huu ni kuwapo kwa sifa ya kisemezano katika kiwango cha kijuujuu (au kwa maneno ya wananaratolojia paramatini, chochote kilicho nje ya matini kama blabu, utangulizi n.k.) kutokana na kuwapo na watunzi wawili katika ukurasa wa hakimiliki, mmoja wa nathari (Zainab Alwi Baharoon) na mwingine wa tungo za kishairi (Ali Saleh) zinazopatikana ndani ya kazi moja ya kifasihi. Katika makala haya tumejaribu kuendeleza mjadala wa usemezano huo katika kiwango hicho, kwa kuonesha ni kwa namna gani inawezekana kudai kuwapo kwa sauti anuwai katika riwaya yenyewe pamoja na dhana nyingine za nadharia hiyo kama utohitimishikivu, mgotanisho wa sauti na mtanziko wa kimaadili. Makala haya yameelekezwa kwenye uwezekano wa kifasiri na kiusomaji wa riwaya hii yanayoweza kukuzwa kwenye tahakiki za baadaye kuhusu riwaya hii na nyingine zenye sifa sawa nayo.

## 1.0 Utangulizi

*Fanani* ni riwaya ya pili ya mtunzi chipukizi wa Zanzibar, Zainab Alwi Baharoon, ambaye ameandika pia riwaya ya *Mungu Hakopeshwi*. Sifa ya kwanza inayoweza kuonekana kwa mara ya kwanza na msomaji katika riwaya ya hii kabla ya kuanza kuisoma ni kuwapo kwa urejeleaji wa watunzi wawili katika ukurasa wa hakimiliki (nathari imeandikwa na Baharoon na mashairi yametungwa na Ali Saleh). Hii ni sifa ya kimajaribio na labda, kwa kiasi fulani, ni uthubutu wa kiubunifu ambao unaakisi msingi muhimu wa mawazo ya Bakhtin unaoeleza kuwa riwaya ni utanzu unaoelekea kukua na unaoweza kuhusisha tanzu nyingine ndani yake, lakini ikabakia kuwa bado ni riwaya. Sifa hii inaiweka riwaya hii katika ngazi hii ya awali kabisa kwenye kile ambacho kinaweza kuelezwa kijuujuu kama ‘riwaya ya ki-Bakhtin’. Kwa kuyatumia mawazo ya mwanafalsafa Martin Heiddegger, tunaweza kusema kuwa msomaji anaanza kuisoma riwaya hii akiwa tayari na uelewa huo wa awali au kwa maneno ya Hans Georg Gadamer, akiwa na ‘upendeleo’ mahususi. Katika hatua hii ya awali, inawezekana kudai kuwa pana sauti mbili zinazoitawala kazi hii katika kiwango hicho cha kiutunzi. Kuwapo kwa

[1] Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Baruapepe: wamitila@gmail.com.

nathari na mashairi ndani ya riwaya hii, kunaweka muktadha na msingi wa aina fulani wa 'usemezano wa kitanzu'. Hii ni sifa ambayo inaweza kuchochea uchunguzi wa kuibuka kwa 'sauti' mbalimbali katika riwaya hii katika viwango tofauti na kuonesha namna mawazo ya Mikhail Bakhtin yanavyoweza kutumiwa kuisoma na kuichanganua riwaya yenyewe.

Katika tahakiki hii fupi, tumejaribu kuonesha ni kwa namna gani mawazo ya Bakhtin yanaweza kutumiwa kama msingi wa uchanganuzi wa riwaya ya *Fanani*. Pia, tumejaribu kuonesha kwamba kuwapo kwa 'vilugha' katika riwaya hii hakuishii tu katika kiwango hiki kilicho bayana, bali kunaweza kubainishwa katika viwango mbalimbali na tofautitofauti vya riwaya hii na kuuchochea mvuto wa kiumbuji wa aina yake. Aidha, tumejitahidi kuangalia ni kwa namna gani usomaji wa riwaya iliyochunguzwa kwa misingi ya mawazo haya, unaweza kutuelekeza kwenye dhana nyinginezo anazohusishwa nazo Bakhtin.

Bakhtin (1981) anaeleza kuwa riwaya inajenga upya wake kutokana na hali hii ya kuwapo kwa aina fulani ya maongezi, mitindo na lugha mbalimbali katika matini ileile moja, ambavyo huelekeza kwenye ukamilifu au umoja wa kisauti. Lugha hizo mbalimbali, kwa mujibu wa mawazo ya Bakhtin, huwa ni mitazamo tofauti ya ulimwengu unaohusika. Bakhtin aliamini kuwa sifa hii ya riwaya ya kuweza kuhusisha lugha na mitindo tofautitofauti huchangia katika kuupa utanzu wa riwaya upekee wa aina yake. Tofauti na Ferdinand de Saussure aliyetofautisha kati ya mfumolugha na udhihirikaji wa lugha hiyo, Bakhtin anashikilia kuwa katika riwaya, lugha si moja bali ni nyingi. Kutokana na usuli huo, kuwapo kwa sauti ya kishairi na kinathari zenye asili tofauti katika riwaya ya *Fanani* kunajenga msingi wa kuwapo kwa aina fulani ya lugha au sauti zinazoshindana au 'taswira za lugha' kama anavyoziita Bakhtin, kila mojawapo ikiwa na mwonoulimwengu, msemaji na muktadha (Bakhtin, 1981).

## 2.0 Muhtasari wa Riwaya

Hii ni hadithi ambayo inaweza kuelezwa kama mfano wa riwaya inayojumuisha sifa za riwaya ya ukuaji na ya kijamii. Hadithi ya riwaya hiyo inawazungukia Rahma na Maimuna, mabinti zake Bi. Zamda ambao wanavutiwa na Vuai, mtangazaji wa habari na mtungaji stadi wa mashairi anayoyaghani katika kipindi cha redio. Mvuto huo unaishia kuwa wa mapenzi ingawa kila mmoja anajaribu kuzificha hisia za moyoni ili mwenziwe asizifahamu. Bi. Zamda anamshuku Vuai, hasa kutokana na sifa alizo nazo kama mwanamume mwenye kiburi na hulka ya kutiliwa mashaka. Hata hivyo, Rahma, binti yake Bi. Zamda, anafanikiwa kumshawishi mama yake kuwaruhusu kuhudhuria uzinduzi wa filamu ya maisha ya Vuai. Kisingizio kikuu anachokitumia Rahma kumshawishi mama yake ni kuwa Vuai ataweza kumsaidia Maimuna ambaye ana kipaji cha utunzi wa mashairi na hata riwaya (ameandika muswada wa riwaya ya *Fumbo*).

Bi. Zamda anakubali "kwa ajili ya furaha ya Maimuna" (uk. 123). Aidha, anaiona hiyo kama fursa ya Rahma kumjua vyema dada yake ambaye anaonekana kuwa mnyamavu na si mwepesi wa kuyaeleza ya moyoni. Bi. Zamda anahisi kuwa Maimuna ana uchungu na ugaga (tajiriba ya uchungu na kuhuzunisha) fulani moyoni, unaotokana na utambuzi wake siku moja kuwa Bi. Zamda si mama yake wa kumzaa. Hali hii inamfanya Maimuna ahisi kama asiyependwa. Baada ya sherehe hiyo, Vuai anaishia kukutana na wasichana hawa na hata kuwaendesha kwa gari lake hadi nyumbani kwa kupitia njia ndefu kwa makusudi. Taswira waliyo nayo Rahma na Maimuna kumhusu Vuai ni kinyume na uhalisi wake kama kiumbe. Vuai anautumia usungo wa wasichana hao kuishia kuwanasa katika mtego wa mapenzi licha ya kwamba mama yao, Bi. Zamda, anawaonya dhidi ya kumwamini na kutekwa na hila zake. Kwa kiasi kikubwa, kichwa cha riwaya anayoandika Maimuna cha *Fumbo* kinaishia kuwa uelekezi wa kiishara wa tabia ya kivutio chao kikuu. Wote wawili, Maimuna na Rahma, wanampenda Vuai ingawa Vuai mwenyewe anaishia kuvutiwa zaidi na Rahma.

Hata hivyo, siku moja Rahma anapompuuza Vuai kwa kumtuhumu dada yake kuwa amemwendea kinyume, Vuai anaapa kulipiza kisasi, jambo linalomchochea Safinia, dada yake wa kazi, kumtafuta Rahma (na hatimaye kukutana na mama yao Zamda) kuhusu uhalisi na tabia ya Vuai (uk. 286). Vuai anaishia kumshawishi Maimuna kuwa na mahusiano naye. Bi. Zamda anafanikiwa kumnasua Maimuna kutoka katika mtego wa Vuai na kuwashawishi mabinti zake kuutambua unafiki na hadaa ya Vuai anayemkabili na kumwonya asiwafuate wanawe. Hadithi inakamilika kwa Rahma, kwa msaada wa Safinia, kuanza biashara ya utarizi na Maimuna kupokea barua ya kampuni ya uchapishaji, Mkuki na Nyota (uk. 360), ya kukubali kuuchapisha mswada wake na Bi. Zamda kuwaelezea wanawe kuhusu mabadiliko ya maisha na jinsi yanavyoathiri uhusiano baina ya mke na mume.

## 3.0 Usemezano, Usauti Uwili katika Mlumbo na Maana

Bakhtin na wafuasi wake wanaiangalia dayalojia kama dhana inayohusisha mapambano kati ya mitazamo (itikadi) mbalimbali. Kinachowasukuma si kuwapo kwa mfanano wa lugha ambao ni aina ya kani kitovu (mvuto wa kuelekea ndani), sifa ambayo ilikuwa msingi wa mawazo ya wana-urasimu wa Kirusi, bali ni kuwapo kwa kani pewa (mvuto wa kutoka nje) zinazokataa kufumbatwa kwenye umoja. Sifa mojawapo inayozungumziwa kama kielekezi cha sauti mbalimbali, ni kuangalia sauti inayotokeza katika shairi, hasa pale wahusika tofauti wanaporejelea shairi ili kuusisitiza ujumbe au mtazamo fulani kama aina ya usemi au mlumbo ambao unawasilishwa bila ya kuwapo kwa viashiria vya moja kwa moja vya unukuzi, yaani kile ambacho kinarejelewa na dhana ya usemi huru taarifa.

Suala lingine linalohusiana na sauti mbili za kisemezano katika kiwango cha uwasilishaji wa simulizi linabainika kwa kuangalia baadhi ya sehemu

zinazohusisha nathari katika riwaya. Zipo sehemu nyingi ambazo tungo za kishairi zinatumiwa kusimulia na kuusisitiza ujumbe unaowasilishwa kwa nathari. Kuna sehemu ambazo msomaji anahisi kuwa kinachofanyika ni aina fulani ya mjalizo wa kisimulizi, ambao badala ya kuwalenga wahusika katika hadithi, unaishia kuwa kama aina fulani ya 'maoni ya kisimulizi' kuhusu kinachowasilishwa. Katika baadhi ya hali hizi, msomaji anaweza kuhisi kuwa kuna kukawizwa kwa mwendelezo wa simulizi kwa kuingiza sifa hii ambayo inaishia kuwa kama 'msimulizi wa pili' (wa kishairi) anayetoa maoni yanayoweza kuwa na maana zaidi kwa msomaji kuliko mhusika au wahusika wanaotagusana katika dayalojia kwenye ulimwengu wa hadithi. Tuangalie mfano ufuatao ambapo Maimuna na dada yake Rahma wanavutana baada ya Rahma kumpuuza Vuai kwa kuhisi kuwa ana uhusiano wa siri na Maimuna:

> Hichi unachokifanya ni zaidi ya kumtukana! Picha gani uliyomuonesha Vuai leo? Kweli umefanya vibaya sana kuliko unavyofikiria! Hakustahiki Vuai kufanyiwa vile ulivyomfanyia! Amejitolea kwa moyo mmoja kutusaidia na wala asitegemee chochote kutoka kwetu, tulimwita akatuitika. Baada ya yote hayo, basi leo ndiyo nawe ukajiona mtu mbele ya watu hata ukafika kuwadharau wale waliokustiri ulipokuwa unatembea peku? Waliokunywisha maji wakati wa kiu? Waliokupa chakula wakati wa njaa, waliokupa hifadhi wakati ulipokuwa na khofu, waliokupa kivuli wakati wa jua kali? Na cha kusikitisha zaidi unawatukana mamba (u)ngali hukuvuka mto. Leo ndiyo shukurani uliyompa Vuai baada ya msaada wake kwetu! Ama kweli shukrani ya punda mateke."
>
> KIPI UTENDEWE
> Kipi sema utendewe     iwe kwako ni ridhaa
> Ni lipi wewe upewe     ambalo litakufaa
> Na ni yepi kwako yawe     moyo wako kutulia
> Kishibe chako kiwewe     tujue yako kinaa
> Sifanye kuwa ni sewe     sifa mbaya kuzagaa
> Kujua wasiyo ndewe     cha siri kutandawaa
> Mateke kurusha wewe     vya watu kuzizengea
> Wajifanya wewe siwe     hisani imepotea
> Hata pishi ujaziwe     mateke warudishia
> Kitaka tena sipewe     ukaja kutulilia
> Na ni ngumu kama jiwe karaha yako tabia
> Ni punda na mkiawe     mekupotea hisia

Baada ya kulitoa lile lililomkereketa moyoni, Maimuna alimwacha Rahma amesimama akiwa bado amezubaa... (kur. 252-253).

Sauti inayowakilishwa kupitia shairi hili inaweza kudaiwa kuujaliza usimulizi kwa kuongeza sifa na ufafanuzi ambavyo havikuwapo katika maneno ya mwanzo ya

Maimuna. Aidha, kuna sehemu ndogo sana inayokuza hoja ya mwisho kuhusu kutokuwa na shukrani. Kwa upande mwingine, kijalizo hicho cha kisimulizi kwa ushairi kinaishia kurefusha matini (na kuongezea wakati-matini ilhali wakati-hadithi unabakia sifuri) kwa namna ambayo hata kama kingeondolewa kisingeathiri mtiririko wa lugha ya kisimulizi. Ikiwa tunakiangalia kama kinachomulika wasifu wa Rahma kama mhusika, basi kinaishia kama aina fulani ya sehemu inayosema zaidi kuhusu mlumbo au diskosi ya kisimulizi (kitu kama aina fulani ya 'meta-diskosi'). Vilevile, inawezekana kudai kwa kutokuwa na maelezo ya ziada (yanayofafanua uelewa wa msomaji kuhusu ulimwengu wa kibunilizi) sehemu hii au 'usimulizi' huo unaishia kuingiza aina fulani ya 'uziada au uradidi wa kisimulizi au hata uziada wa ndani-matini'.

### 3.1 Mgotanisho na Sauti Huru

Kuwapo kwa 'sauti' ya kishairi na ya kinathari katika usimulizi wa riwaya ya *Fanani* kunatuchochea kusema kuwa kuna aina fulani ya uwekaji sambamba au mgotanisho wa sauti mbili (pengine zilizo huru) katika usimulizi wa hadithi iliyopo. Japo tungo za kishairi zinatumiwa kwa aina fulani ya mjalizo wa maelezo ya kinathari, kuna sehemu ambapo msomaji anahisi kuwa sauti ya kishairi ina jukumu la kisimulizi pia. Hali hii inatokea pale ambapo msomaji anahisi kuwa kupitia sehemu hiyo ya kishairi, kuna ufafanuzi na maelezo au ziada ya kihusika au kidhamira yanayopatikana. Sauti hiyo 'mpya' ya kisimulizi inayosikika, inaishia kuwa aina fulani ya usemi huru taarifa (au hata mawazo huru taarifa).

### 3.2 Heteroglosia/Wingilugha na Mivutano ya Ndani kwa Ndani

Dhana ya heteroglosia au wingilugha inatumiwa na Bakhtin kuelezea kuwapo kwa aina tofautitofauti za sajili za kijamii (au hata wakati mwingine lugha) katika matini. Bakhtin (1984) anaiangalia riwaya kama utanzu wa kielelezo cha wingilugha/heteroglosia. Kwa maoni ya Bakhtin, dhana ya wingilugha ni kitambulishi kikuu cha lugha ya riwaya; pia, ni mojawapo ya misingi mikuu ya kuitofautisha lugha hiyo na lugha kama vile yaushairi. Kwa maoni yake, zipo mbinu kuu nne ambazo hutumiwa kama msingi wa kuhusisha na kuingiza sifa hii ya wingilugha au heteroglosia katika riwaya. Mbinu hizo ni: usemi halisi wa mhusika wa kifasihi, uwasilishaji wa nafsi ya tatu wa usemi wa ndani wa mhusika, 'umtindoishaji' na uingizaji wa tanzu nyinginezo za kifasihi kama vile hurafa au ngano, nyimbo na ushairi katika matini. Kwa kuongozwa na msingi wa mawazo ya Bakhtin, tunaona kuwa riwaya ya *Fanani* imesheheni uingizwaji wa utanzu mwingine (kwa kuwapo kwa tungo za kishairi), matumizi ya usemi halisi wa wahusika na, kwa kiasi kikubwa, kuwasilisha mawazo ya ndani ya wahusika, hususani kwa matumizi ya usemi huru taarifa kwa namna tofauti kama vilekupitia tungo za kishairi zinazotumiwa.

Tunapoichunguza riwaya hii kwa umakini, tunaweza kubainisha hali ambapo utungo wa kishairi unaishia kuwasilisha usemi wa mhusika anayehusika katika

njia isiyokuwa ya moja kwa moja, yaani kile ambacho Cohn anakieleza kama 'monolojia iliyosimuliwa' (Cohn, 1978: 99). Ufuatao ni mfano huo:

> Alilala chali mikono yake ameikunja nyuma ya kichwa chake, macho aliyafunga ili kuruhusu ubongo wake kupumzika. Kama mkanda wa filamu ilimpitia sura ya Rahma na tabasamu lake...
>
> UZURI WA MACHO YAKO
> Hakika Mola amekupendelea
> Kilicho chema amekuchagulia
> Macho mazuri amekujalia
> Kakupa kwa kheri ya kuyatumia
> Uzuri wako kuukamilishia...
> (uk. 175).

Katika mfano huu (na katika miktadha mingine pia), msomaji anahisi kuwa utungo wa kishairi unaoingizwa katika simulizi unaishia kuwa kile ambacho Genette anakielezea kama 'diskosi/usemi uliosimuliwa', pale ambapo kauli au matamko ya mhusika (anayenukuu shairi) yanawasilishwa. Hali hii tunaiona na kuihisi pale ambapo utungo wenyewe unaingiliana na kuwiana kwa njia ya moja kwa moja na usimulizi uliotangulia.

Katika baadhi ya miktadha, msomaji anapata hisia ya kuwa utungo wa kishairi hautekelezi jukumu la kuwasilisha sauti inayojibu au kushiriki katika mazungumzo au usemezo na wahusika wengine katika ulimwengu wa hadithi, bali ni kama sauti nyingine ya kisimulizi. Kwa msingi huu, msomaji anapata hisia ya kuwapo kwa sauti nyingine inayosimulia au aina fulani ya 'msimulizi mbadala'. Hii ni hali ambayo kwa namna fulani inaishia kujenga uhusiano au hata usemezano kati ya matini na msomaji wa matini yenyewe. Tuangalie mfano ufuatao:

> Na ukiila ikakudhuru utakuwa hukuitendea haki nafsi yako, maana hakuna mwenye haki ya kuidhuru nafsi yake wala ya mwingine! Kilichokuwa haramu kwako hakitakuwa haramu kwa watu wote.
>
> HALALI KWAKO HARAMU MWINGINE
> Kisicho chake usile japo ukakikamia
> Ukione vilevile masafa kukiwekea
> Sijifanya duduvule kawa ni kupekecheua
> Kibivu hata kiweje kuiva kitakavyokua
>
> Kizuri kipendezaje jamili kikivutia
> Sikile hata iweje kwako ni haramu kuwa
> Gharama ukitolee kukuza na kukilea
> Wajibu wako ujue chako kukihudumia

Malipo sitarajie eti kwamba kimememea
Kwa mbali nacho simama hata kukikaribia
Usione cha mkoma Bongoni sijewazia
Uweze wako mtima makosani sijeingia

Chako kilicho haramu ni halali kwa mwenzio
Sijitie nyingi hamu ukayaona ya leo
Utaingia wazimu utembee bila nguo

"Siku zote using'ang'anie kitu kilichokuwa hakipo sawa kwako, eti umeona kwa mwengine kimekwenda vizuri (uk. 239).

Katika mfano huu, shairi linatekeleza majukumu ya aina mbili. Kwanza, linafanya kazi kama nyongeza ya kisimulizi kwa kutoa maelezo ya ziada kwa namna ambayo inamfanya msomaji kuhisi wakati-matini unaoongezwa. Kwa upande mwingine, kuna hisia kuwa ushairi huu unaishia kuwasiliana zaidi na msomaji kutokana na sifa yake ya kutojifunga zaidi kwenye kauli inayotangulia au hata kufuatia utungo huo.

### 3.3 Mhusika na Sauti: Ukanda wa Mhusika

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), mhusika katika riwaya huwa na …ukanda wake mwenyewe, eneo lake la mamlaka juu ya muktadha wa kiuandishi, eneo ambalo aghalabu linakwenda mbali sana na mipaka ya mlumbo halisi anaopewa kama mhusika (uk. 320; tafsiri ya mwandishi wa makala). Ukanda wa mhusika hujengwa au huundwa na milumbo au diskosi ya wahusika kutokana na njia fiche, yaani zisizokuwa wazi za uwasilishaji usemi kama maneno na misemo ambayo husambazwa kwenye usemi kupitia udondoshi, maswali, mishangao na elementi nyingine ajinabi ambazo huingilia sauti ya mwandishi. Kanda za wahusika hazitilii maanani milumbo ya wahusika pekee, bali huwazia pia sifa nyinginezo za kuwako kwa wahusika hao. Sifa hiizo ni kama usuli wa wahusika hao, mikabala ya wahusika wengine pamoja na mkabala wa msimulizi kuwahusu na pamoja itikadi zao.

Msomaji wa kazi ya kifasihi huunda na kujenga utambulisho wa mhusika, siyo tu kutokana na maelezo ya moja kwa moja, matendo yake au unukuzi wa usemi wake (au sauti yake), bali pia kutokana na ukanda wake mpana wa mdokezo wa kiusemi. Ukanda huu anaouzungumzia Bakhtin ni aina fulani ya ukanda wa athari unaoweza kuathiri na kuingilia kanda nyinginezo. Mhusika huwa ni aina fulani ya makutano na chanzo cha sauti za kijamii katika matini. Ukanda wa mhusika unabainika vizuri pale ambapo sauti ya mhusika inaingiliana kwa namna fulani na sauti ya mwandishi na wakati mwingine kuipinga kama ambavyo tunaona mara kadhaa katika riwaya ya *Fanani*. Hayo yanadhihirika katika mfano ufuatao:

> "Haya twende zetu tusizidi kukawia," Bi. Zamda alitoa maelekezo. Bila ya kujibu kitu Maimuna alimfwata Bi Zamda nyumanyuma. Rahma aliwasindikiza kwa macho kisha akashusha pumzi ndefu, akajisemea rohoni. "Ah, mbona mambo? Na miye ndiyo kwanza natafuta safari ya kumtafuta Vuai, naanzia wapi? Ah, liwe na liwalo tutajificha ndani mpaka lini? We sema lakini yanainhggia huku yanatokea kule. Miye hapa Vuai ndiyo mpango mzima," alisema Rahma kimoyomoyo na akijulia hilo angesikia Bi. Zamda pangemka Vita vya Tatu vya Dunia.
>
> MOYO WANGU WAZI
> Moyo wangu uko wazi ndanimwe ukaribie
> Usisite laazizi kwa nje usiiisie
> Ufanya yako makazi Haraka uje uhamie
> Karibu habibi
> Habibi karibu
> Usijione mgeni utakalo niambie
> Nikubebe vitangani aula nikupepee
> Kwa sauti ya laini utakalo jisikie…
> (kur. 23-24).

Inawezekana kudai kuwa sauti ya Vuai katika shairi hili inatekeleza dhima ya kisimulizi. Kwa msingi huu, inachukua kanda mbili:ukanda wa Rahma kama mhusika na ukanda wa msimulizi wa kubainisha yanayompa Rahma moyoni. Katika riwaya hii, Rahma anakuza ukanda wake kwa kuwapo hata kwa maneno ya kihisia kama "he maa wee" (uk. 25) ambayo Bakhtin anayataja kama viashiria muhimu. Kwa mtazamo wa Bakhtin, hatupaswi kuiangalia riwaya kama usemezano baina ya mwandishi na msomaji tu aukama inayohusisha mabadilishano baina ya nafsi za kisemezano zilizopo katika matini yenyewe. Bakhtin hamwangalii mhusika kama mtu tu kama ilivyotokea katika mikabala ya zamani ya mhusika, bali kwake mhusika huwa ni 'sauti' zilizomo kwenye matini.

## 4.0 Migogoro na Upinzani wa Kifasihi

Miaka mingi iliyopita, Marx na Engels, katika *The Communist Manifesto* walitoa kauli maarufu kuwa historia ya jamii ni historia ya mapambano baina ya matabaka. Bakhtin analiendeleza wazo hili kwa namna fulani lakini badala ya kuzungumzia matabaka mawili tu kama walivyofanya Marx na Engels, anaibainisha migogoro na harakati nyingi; baadhi kubwa na nyingine ndogo mno, na hata nyingine katika makundi yenyewe.

Katika baadhi ya mifano hii, inawezekana kudai kuwa tungo zinazoingizwa ili kuwa aina ya jibu/mrejesho wa mazungumzo ya mhusika anayezungumza na anayejibiwa kwa utungo huo, zinaelekeza pia kwenye aina fulani ya mvutano wa ndani kwa ndani (kwa upande wa msemaji) ambao anaamua kumshirikisha

mwenzake. Mfano mzuri unatokea pale ambapo Maimuna anawasilisha mawazo yake katika kipindi cha Vuai baada ya Vuai mwenyewe kughani shairi. Kinachotokea hapa ni aina ya usemi/mlumbo kinzani.

> "Naam Maimuna unataka kumuuliza nini fanani."
>
> "Sina suala ila nataka kumpa burudani tu kama vile atupayo yeye," alizungumza kwa kujiamini.
>
> "Naam tupe. Fanani anakusikiliza," Vuai lilimtoka tabasamu.
>
> DUNIA TAKUHUKUMU
> Ulifanya sirini    lakini hukutosheka
> Na pia ya hadharani   hata sifa ulitaka
> Kama kama hayawani  kigoma ukatimika
> Bilisi kakuzaini    hukuijua mipaka
>
> Kutafuna vifaranga   makoo ukiyasaka
> Makusudi ukalenga    kwa ulipoaminika
> Katumia umalenga    mitego yako kuweka
> Ukazidisha ujinga   tamaa ikakuteka
>
> Kitu hukukibakisha   rekodi ukaiweka
> Ikawa hadi watisha    mbali watu kukuweka
> Vitaa ukasafisha     muhuri ukabandika
> Ukaapa utavisaha  vyote vilivyohusika
>
> Takulipa Rabi Mola    dua zikija alika
> Vyote ulivyokula  naapa tavitapika
> Wala hakuna aula   hilo nakupa hakika
> Uliowapa madhila   nao watakuja cheka
>
> Kiitikio:
> Vituko ulizidia ukadhani utadumu
> Dunia hukuijua itarudisha hukumu.

Kwa kumchukulia Vuai kama kiwakilishi cha tabaka la wanaume ambao katika jamii wanasawiriwa kama wenye mtazamo wa kiudhalilishaji dhidi ya wanawake, utungo huu wa Maimuna unaishia kuwa na mchango muhimu katika kuuakisi mvutano wa kisemezano aliouzungumzia Bakhtin. Si tu mvutano baina ya sauti yake na ile ya Vuai, bali pia baina ya sauti anuwai katika jamii ambazo zinadhihirishwa na kauli, maneno, maadili na hali tofautitofauti, kama vile inayomhusisha Salama, mama mzazi wa Maimuna. Katika mtazamo tofauti, hii ni

sifa inayoakisi ujibikifu[2] wa riwaya hii katika muktadha mpana wa wanajamii, wasomaji na maisha ya jamii ya mtunzi.

**5.0 Itikadi, Utambulisho wa Kisemezano na Ujumi na Usomaji wa Riwaya**
Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), itikadi huwa ni mlumbo au diskosi ya watu wengine ambao hujaribu kuyadhibiti mahusiano yetu na ulimwengu, yaani ule msingi wetu wa tabia au hulka. Kwa maoni yake, maneno yanayorejelea maadili ya kikaida au maneno ya mzazi ambaye ana mwelekeo wa mtazamo wa kihafidhina, ambao unachukua umbo la usemi au mlumbo wa kimamlaka, ni mfano wa itikadi. Bi. Zamda, kwa mtazamo wa wanawe, Rahma na Maimuna, ni kielelezo kizuri cha anachokielezea Bakhtin. Tuangalie mfano ufuatao:

> "Rahma mwache mwenzio. Kwani kilichokuamsha ni nini hasa? Hebu kalale usije kutuamkia saa kumi jioni!" alikaripia Bi. Zamda.
> "He, maa wee!" Rahma amekasirika kauvuta mdomo ukawa kama wa bata.
> "He! Ina maana hatokwenda kulala yeye?" aliuliza kwa mastaajabu.
> "Mpaka lini utashindana? Yeye ana kazi yake anafanya, wewe unafanya nini? Hebu kalale huko usinipigishe kelele saa hizi!" Bi Zamda kakasirika. "Na ole wako uchelewe kuamka kesho, maji utaita mma! Hukunijua bado…
> "Haya maa njoa malizia kazi yako achana naye huyo," aliamuru
> "Mwanga!" Rahma alisema kwa kejeli…
> "Rahma nitakutia makofi nakwambia. Kalale mwache afanye kazi yake. Mbona kisirani wewe?"
> "Kwani nikikaa naye itakuwa nini?" (uk. 56).

Katika riwaya hii, siyo tu sauti za Rahma na Maimuna ndizo zinazolenga kupinga na kuiumbua itikadi na mlumbo tamalaki wa Bi. Zamda na tabaka analowakilisha, bali pia tungo za kishairi za Vuai wanazozisikiliza na kumkariria mama yao na hata tungo za Zamda mwenyewe anazozitumia kujibiza misimamo yao (kwa mfano, kama inavyotokea kwenye mwendelezo wa mazungumzo yaliyonukuliwa hapo juu (kur. 55-59). Kwa mujibu wa Bakhtin, itikadi huweza kudhihirika kupitia mlumbo/usemi shawishi wa ndani ambao tunauchagua kwa hiari (bila ya kulazimishwa).

Suala ambalo linatushughulisha hapa kama wasomaji wa riwaya hii ya *Fanani* ni kubainisha namna ambavyo tunaweza kusema riwaya hii inahoji umonolojia na

---

[2] Bakhtin anaitumia dhana hii kuelezea kuwa matendo ya mtu hutokea katika muktadha ambapo wengine huwa na mrejesho kuyahusu. Neno hili limetumiwa katika kitabu hiki kama fasiri ya dhana ya '*answerability*'.

kudhihirisha mapambano ya milumbo au diskosi shawishi kati ya na miongoni mwa watu (wahusika) binafsi. Je, ni kwa kiasi gani, kwa kuangalia mazungumzo baina ya Rahma, Maimuna na Bi. Zamda, tunaweza kusema kauli na maneno ya Rahma na Maimuna (na hata wakati mwingine sauti ya kujibiza au ya kusema tu '*Maa...*' bila ya kuongeza mengine) inatuelekeza kwenye aina fulani ya upinzani wa itikadi inayowakilishwa na mtazamo wake kuhusu mkabala wake kama mwanajamii anayewakilisha tabaka fulani kuwahusu watoto wa kike na kuhusu matarajio ya kijamii?

### 5.1 Usemezano wa Kitanzu na Utatizaji wa Kimaana

Katika sehemu iliyotangulia, tumedokeza kuwapo kwa usemezano wa kitanzu katika riwaya hii kunakosababishwa na kuwapo kwa nathari na ushairi kwa mapana. Suala ambalo linaweza kumshughulisha mhakiki ni kama usemezano huo unakamilisha na kuwezesha uwasilishaji wa kimaana au unatatiza kwa kuvuruga muumano wa kimaana unaojengwa na mtiririko wa kinathari kama kwa kuingiza wizani wa kishairi (na mtiririko tofauti), maana inaishia kutatizwa. Kwa mfano, je, vichwa vya mashairi yanayopatikana katika riwaya vinajaliza, kuumbua, kukamilisha au kudengua yanayosimuliwa kabla na baadaye? Yamkini hili ni swali la mjadala ambalo msomaji anaweza kulifuatilia, na ambalo kazi nzuri ya kifasihi hudhamiria kuchochea.

Inawezekana kudai kuwa katika baadhi ya miktadha tungo hizi za kishairi na mada zake zinaelekea kukinzana na mkondo wa simulizi kwa kuingiza sifa ambayo kwa kiasi fulani inatengua umakini wa msomaji kuhusu kilichokuwa kinaendelea, na kwa kiasi huishia kuwa kama aina fulani ya tahakiki (metatahakiki) ya kilichotangulia. Hii ni sifa ambayo inachimuzwa na inayomfanya msomaji kuhisi kuwautunzi wa mashairi umefanywa na mwandishi tofauti na aliyeandika nathari. Kielelezo kizuri cha hali hii kinapatikana pale ambapo Bi. Zamda anazungumzia kuhusu suala la mtazamo wa mwanamke na misukosuko yake katika jamii ya sasa, kisha shairi kuhusu 'Mwanamke ni Vazi' (uk. 347) likachopekwa ndani. Kuna aina fulani ya utoupatanifu katika sehemu hii. Hata hivyo, sifa hii inakuwa kielekezi muhimu kuhusu suala la kuwapo kwa sauti huru tofauti ndani ya riwaya hiyo.

## 6.0 Utohitimishikivu na Mtanziko wa Kimaadili kwa Wahusika

Bakhtin (1984) alibainisha kuwa neno huwa na uwazi fulani. Anaeleza kuwa hamna chochote cha ki-uhitimishikivu ambacho kimetokea ulimwenguni, neno la mwisho la ulimwengu na kuuhusu ulimwengu halijasemwa bado. Ulimwengu ni wazi na huru, kila kitu kipo katika wakati ujao na kitaendelea milele kuwa hivyo" (Bakhtin, 1984: 166). Hali hii inatokana na ukweli kuwa, kila neno au kauli inayosemwa huwa inachochea neno, yaani kauli au tamko jingine la kujibiza au kuipa mrejesho. Majibu hayo nayo huwa na sifa hiyo hiyo kiasi cha kwamba unajengwa aina fulani ya mkufu. Dhana ya utohitimishikivu hurejelea aina fulani ya mvutano ambao huwapo baina ya uwazi na uhatima. Mtazamo huu wa

utohitimishikivu wa neno au kauli unaweza kutumiwa katika kuwachunguza wahusika wa kifasihi. Ikiwa tutaihusisha dhana hii na wahusika, tutaelekea kusema kuwa hakuna mhusika (au hata matini) anayeweza kueleweka au kufasiliwa kikamilifu. Je, ni kwa kiasi gani tunaweza kusema kuwa dhana ya utohitimishikivu kuhusiana na wahusika inabainika katika riwaya ya *Fanani*? Mmojawapo wa wahusika wanaoakisi sifa hii, hasa katika sehemu za mwanzoni ni Maimuna, dada yake Rahma na mwanaye (asiye wa kuzaa) wa Bi. Zamda. Je, katika riwaya hii Maimuna ni mwathirika wa yanayotokea (anayepembezwa jinsi mwenyewe anavyolalamika), au hila za Vuai, hasidi au mbabe? Hii ni sifa inayoelekeza kwenye utohitimishikivu fulani wake kama mhusika katika riwaya hii.

Kwa upande mwingine, dhana ya mtanziko wa kimaadili anayoizungumzia Bakhtin inaweza kutumiwa kuwarejelea wahusika kadhaa, hususani Rahma, Maimuna na Vuai na labda kwa kiasi fulani Salama. Dhana hii kimsingi inalenga kubainisha au kuonesha namna ambavyo mhusika anaweza kuwa 'mwenye maadili' na 'asiyekuwa na maadili' kwa wakati huo huo. Mtazamo huu unatuwezesha pia kuonesha au kudahili namna ambavyo mhusika anaweza kuoneshwa kama mwenye maadili licha ya kwamba ameyatenda maovu fulani. Je, ni kwa namna gani tunaweza kumtazama Maimuna anayeuchukua msimamo tofauti na matarajio ya mama yake, Bi. Zamda, na utamaduni wake kama mwenye maadili? Swali hilo linaibuka kutokana na kitendo hicho kuwa msingi wa ung'amuzi wake na utambuzi wa umuhimu wa kumkabili Vuai mwenyewe na kujielewa na kuielewa jamii yake. Je, msukumo wa Rahma, dada yake, kufanya juu chini kumtembelea Vuai ambaye ni fasiki na mdanganyifu na kuishia kwa dada yake Maimuna kuyapata maarifa muhimu kuhusu uandishi wake unaoishia kwenye kukubaliwa kwa muswada wake wa kitabu na Mkuki na Nyota ni sifa inayoweza kufasiriwa katika kiwango cha kimetabunilizi? Vipi kuhusu kitendo cha Salama, mama mzazi wa Maimuna, cha kumtelekeza Maimuna baada ya kumzaa (tendo la ukosefu wa maadili) kwa rafiki yake, Bi Zamda, na kuishia kulelewa pamoja na Rahma (ili awe na dada) na Bi. Zamda anayempenda kama mama yake? Baadhi ya maswali haya yanatuelekeza kwenye mawazo ya Bakhtin kuhusu ujumi na hasa umahususi na upekee kuwa kila binadamu anapaswa kutathminiwa na kuhukumiwa katika muktadha wa umahususi wake.

**7.0 Hitimisho**

Katika tahakiki hii fupi, tumeona jinsi ambavyo riwaya ya *Fanani* ya Zainab A. Baharoon inavyoweza kusomwa kwa misingi ya mawazo ya Mikhail Bakhtin. Imebainisha namna ambavyo kuwapo kwa tungo za kishairi, ambazo katika riwaya zinahusishwa na mhusika Vuai, zinavyoweza kutazamwa kama aina ya sauti inayotumiwa au zinazotumiwa na Rahma na Maimuna kwa namna kuu mbili. Kwanza, zinatumiwa kama sauti za kupinga na kuumbua sauti kuu inayotamalaki ya mama yao, Bi. Zamda, ambaye anatamani waishi na watende mambo kwa namna fulani mahususi inayohusiana na jamii yake iliyomkuza yeye kama

mwanamke. Kwa kiasi fulani, sauti hizo zinaishia kuidengua satua ya utamaduni huo ambao kwa kiasi fulani, ni utamaduni unaohusishwa na mfumo wa ubabedume ambao kwa maoni yao unamtumia mama yao kama chombo cha kuuendeleza (katika sehemu kadhaa anamrejelea mumewe ambaye amekwisha kufariki). Pili, ni sauti ambazo zinaelekeza kwenye 'ukombozi' wa kizazi chao kama wasichana wa jamii ya kileo, wa jinsi ya kufurahia na kuufurahia uhuru wa uamuzi na kwa kiasi fulani msingi wa utambulisho wao.

Sifa mojawapo kuu ambayo imeibainishwa na kusisitizwa ni kuwa, utumiaji wa utanzu wa kishairi katika riwaya hii unaingiza sifa ya usemezano katika kazi yenyewe. Bakhtin aliamini kuwa ili kazi iweze kuelezwa kama ya kipolifoni, sharti wahusika waepuke kuwa chini ya udhibiti wa kiuandishi au aina yoyote ile ya mlumbo au diskosi ya kimonolojia. Hii ni sifa ambayo msomaji anahisi ipo, japo ni kwa kiwango fulani katika riwaya hii.

Kwa kumalizia, tunaweza kusema kuwa ujumuishwaji wa ushairi na nathari katika riwaya hii, ambayo ni sifa ya kimajaribio (hasa kwa sifa yake ya kuhusisha tungo za kishairi za mtunzi mwingine) kwa kiasi kikubwa, umemwezesha mwandishi kuigiza kisanaa jadi ya usemezano wa kingonjera katika jadi ya jamii zetu kwa namna ambayo inaifanya riwaya hii ilete pamoja sauti mbalimbali zinazosemezana, na kumfanya msomaji avute taswira ya muktadha wa majibizano unaohusisha wasanii mbalimbali. Mwisho wa riwaya unaelekeza kwenye utohitimishikivu mkubwa wa kiuhusika, sifa ambayo inawezekana kudai, inaelekezwa na hata kichwa cha riwaya kinapoangaliwa katika muktadha mzima wa ulimwengu wa kibunilizi.

**Marejeleo**

Baharoon, Z. A. (2022) *Fanani*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Bakhtin, M. M. (1981) *The Dialogic Imagination*. Four Essays. Carl Emerson & Michael Holquist (waf). Austin: University of Texas.

Bakhtin, M. M. (1984) *Problems of Dostoevsky's Poetics*. Trans Caryl Emerson. Minneapolis: University of Minnesota.

Bakhtin, M. M. (1990) *Art and Answerability*: Early Philosophical Works by M. M. Bakhtin. Michael Holquist and Vadim Liapunov (edrs.) Austin, TX: University of Texas Press.

Cohn, D. (1978) *Transparent Minds*. Narrative Modes for Presenting Consciousness in Fiction. Princeton/New Jersey: Princeton University Press.

Holquist, M. (2002) *Dialogism. Bakhtin and His World*. London and New York: Routledge.

Pearce, L. (1994) *Reading Dialogics*. London: Edward Arnold.